


IWE NURU



**Mtu hataishi kwa
mkate tu, ila kwa
kila neno litokalo
katika kingwa cha
Mungu.**

Mathayo 4:4

Mchungaji wa kanisa hili, Julio Villar, alisikia kwa mara ya kwanza ujumbe wa wokovu katika redio alipokuwa katika baa. Aliwaacha rafiki zake pale ndani ya baa na akaanza kutafuta kanisa lililotangaza kipindi hicho. Aliingia kanisani humo na akasikiliza mahubiri. Kisha alimpokea Yesu kama Mwokozi wake siku iliyofuata. Alisoma Agano Jipya lote kwa wiki moja. Kisha alianza kushuhudia na kuhubiri hata ingawa hakuwa amefundishwa.

Baadaye Villar alijiunga na chuo cha Kibatisti cha seminari katika nchi ya Argentina. Alikuwa mchungaji katika kanisa mojawapo la huko. Alitaka sana kurudi kwao Peru, lakini hakuwa na pesa za kutosha kusafiria. Kisha siku moja akaalikwa kuja kuhubiri Peru katika mkutano wa ufufuo. Kanisa la Central walimwita aanze kuwa mchungaji wao.

Kwa sasa Villar ni mkurugenzi wa huduma ya umisheni katika Jumuia Kuu ya Wabatisti wa Peru na pia mchungaji. Peru ina Wamisheni sita ambao ni wenyeji wa nchi hiyo. Wanao pia wamisheni kutoka Amerika, Brazil, na Argentina wanaojitoa kusaidia watu wa nchi hii kujua Bwana Yesu Kristo.

SEHEMU YA' NNE: Wabatisti wa Cajamarca

Cajamarca ni mji mwingine ulioko Peru. Uko katika milima ya Andesi

yenye urefu wa futi elfu kumi. Wamisheni wa Kibatisti wanajenga mifereji ya kutoa maji milimani na kuyaelekeza katika sehemu kame za nchi hiyo. Wamemaliza sasa kujenga mifereji mitatu. Jamaa wapatao mia tatu sitini watapata maji ya kutumia kwa ukulima.

Wamisheni huwa wanawashuhudia watu katika sehemu hizi wanazojenga mifereji. Makanisa ya Wabatisti yameanzishwa katika miji hii iliyo karibu na mifereji hiyo: Cajamarca, Ramada, na Matara.

KIONGOZI

Mtu huwa na maisha mapya na matumaini mapya ya kesho anapompokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wake. Wachungaji, wamisheni na washiriki wa makanisa wa Peru wanawapa wengine matumaini wanapojitahidi kushuhudia kwa njia nyingi tofauti.

Peru iko mbali na nchi yetu, lakini ujumbe wa Injili ni mmoja. "Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa Bwana, kama maji yaifunikavyo bahari" (Habakuki 2:14). Tunatumaini kwamba Peru itajazwa na maarifa ya utukufu wa Bwana wetu.

MAOMBI

IWE NURU

Mwandishi: Mrs. Roy Davidson

Masomo Kwa Mikutano ya Wanawake

Africa Coordinated Curriculum for Women

Co-Lit 2-2-3

Published and Printed by
Baptist Publications House
Box 30370, Thika Road, Nairobi

© Copyright, 1990
Baptist Publications House
All rights reserved

ya Kihindi wanaishi katika sehemu za misitu.

Mji ulio mkuu Peru ni Lima. Watu wapato milioni tano wanaishi katika mji huu wenye kiangazi ambao ni mkubwa kuliko mji wa Nairobi. Magari ya moshi na motokaa ya abiria huwaleta watu wengi kuishi mjini Lima kila siku. Hujenga nyumba za muda kwa kutumia miteka na nyasi. Unaweza kuona katika sehemu zingine za Lima nyumba kubwa, makanisa mazuri ya kikatoliki, na nyumba za kuhifadhi vitu vya kale vya Wahindi wa Inca.

Kundi la waasi litwalo "Sendero Luminoso" (Njia ya mwangaza) ndilo linalosumbua nchini Peru. Waasi hawa wananuia kuipindua serikali. Wao hujaribu kutupia makomboro vituo vya polisi, Kambi za jeshi na sehemu zingine muhimu. Lakini watu wa kawaida hushughulika na kazi zao za kila siku bila shida wala kusumbuliwa.

SEHEMU YA PILI: Makanisa Yaliyoko Lima

Mchungaji Juan Armas ana matumaini makubwa na Kanisa la Wabatisti litwalo Mto wa Mungu (Divine Springs). Kanisa hili lina shule ya watoto wadogo na linatumainia kuwa na shule ya msingi. Wameanzisha kanisa lingine linaloitwa Safina ya Nuhu. Kanisa la Mto wa Mungu linatumaini kwamba vituo vitatu walivyoanzisha vitakuja kuwa makanisa. Armas huwafundisha washiriki masomo ya TEE ili waweze kusaidia kuanzisha makanisa mapya. Jengo la Mto wa Mungu ni la orofa moja. Lakini kuna matumaini ya

kuongeza zingine mbili wakati washiriki na makadirio yao yanapongezeka.


Kanisa hili lina mradi wa kuwalisha watoto maskini. Mchungaji ana matumaini ya kuanzisha kiwanda cha mikate ili kuwapatia watoto hawa mikate. Anataka kununua shamba na kupanda mboga za kuwalisha watoto hawa. Mradi huu pia utawawezesha washiriki wa kanisa kupata kazi. Mipango mingine ya kuwasaidia washiriki wapate kazi ni: kununua mtambo wa kushona fulana ili wanawake washone na kuziua, na kutumia ujuzi wa wanaume wa kujenga nyumba.

Mji wa Lima una makanisa ishirini ya Kibatisti na vituo thelathini na nane za kuhubiri. Makanisa mengine ya Kibatisti husaidia jamii zao kwa kuanzisha kliniki za madaktari, na kufundisha ushonaji na aina ya chakula bora. Mchungaji mmoja huwafundisha vijana jinsi ya kutengeneza saa zilizoharibika. Kanisa lingine huwafundisha wanawake jinsi ya kushona miteka.

SEHEMU YA TATU: Central Baptist Church Lililoko Trujillo

Kanisa kubwa sana la Kibatisti lililoko nchini Peru ni Kanisa la Kati (Central Baptist Church) ambalo liko katika mji wa Trujillo. Kanisa hili lina washiriki 625 na vituo sita vya kuhubiri. Shughuli hufanyika hapo kanisani kila siku: huwa kuna ushirika wa wanawake, mikutano ya vijana, maombi na masomo ya Biblia au ushirika wa udugu.

Bahari ya
Pasifiki



YALIYOMO

MANENO MAKUU YA BIBLIA

Mwandishi Mrs. Roy Davidson

1. Hapo Mwanzo - Mwanzo 1
2. Mchungaji Mwema - Zaburi 23
3. Mtumishi Mwenye Huzuni - Isaya 53
4. Baba Mwenye Pendo - Luka 15:11-32
5. Njia Yenye Furaha - Mathayo 5:1-12
6. Jinsi ya Kuomba - Mathayo 6:5-13
7. Njia Kweli na Uzima - Yohana 14:1-15
8. Zaidi ya Washindi - Warumi 8:28-30
9. Amani ya Mungu - Wafilipi 4:4-9; 12-13; 19-20
10. Njia ya Upendo - 1 Wakorintho 13
11. Mwaliko Mkuu - Isaya 55:1-3; 6-9
12. Kristo Aleta Tumaini Peru
Mwandishi: - J. Carter

KRISTO ALETA TUMAINI PERU

Kilini cha Masomo: Maneno Makuu ya Biblia

Kuyasoma Maandiko: Habakuki 3:17-19

Kifungu cha Kukumbuka:

"Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa Bwana, kama maji yaifunikayo bahari."
Habakuki 2:14

KIONGOZI

Ni kazi kubwa sana kuwapikia watoto 150 chai ya asubuhi! Elva Chuquitape wa kanisa la Kibatisti katika mji wa Lima, Peru, alifanya hivyo kwa miaka mitatu. Aliwapikia pia chakula cha mchana. Kanisa ndilo lilitoa chakula cha kuwapa watoto hao. Elva alipika bila ya kulipwa. Yeye alijitoa kupika.

"Ilikuwa njia ya kumtumikia Bwana," akasema Elva.

Elva hakuwa Mkristo miaka minne iliyopita. Yeye na mumewe walikuwa na shida nyingi katika ndoa yao. Jirani yao aliwatembelea na akawaambia habari ya Yesu. Elva hakushughulika wakati ule. Baadaye mumewe Elva alimwacha pamoja na wanawe watatu. Elva alishikwa na hofu na akamwambia jirani yake ampeleke kanisani. Kanisa la Kibatisti lililokuwa karibu, lilikuwa na mkutano wa Uinjilisti, naye Elva akampokea Yesu kama Mwokozi wake usiku huo.

Elva hupata pesa za kuwalisha wanawe kwa kuwaoshea watu wengine nguo au kuwafanya usafi nyumbani kwao au kushona. Lakini alijitoa

kuhudumia kanisa hadi washiriki wengine walipoanza kumsaidia.

Ni jambo la muhimu kwa makanisa ya Peru kuwasaidia watu kumjua Yesu na kuishi maisha mazuri. Tutajifunza leo kuhusu Wabatisti wa Peru na matumaini wanayotelea watu kupitia kwa Yesu Kristo.

SEHEMU YA KWANZA: Nchi ya Peru

Peru ni nchi iliyoko kusini mwa Amerika. Bahari ya Pasifiki iko upande wa magharibi mwa Peru na nchi ya Brazil upande wa mashariki. (Tazama ramani.) Nchi hiyo ni kavu upande wa pwani. Milima mikubwa inatenganisha sehemu kavu na sehemu ya misitu mwenye mvua nyingi.

Hapo kale Wahindi wa Inca walikuwa wameendelea sana huko Peru. Walikuwa na serikali imara na dhahabu nyingi. Hatimaye Wazungu wa Uspania walifika katika nchi ya Peru na kuwashinda. Wengi wao waliwaoa Wahindi hao. Lugha inayosemwa Peru siku hizi ni Kiispania. Wahindi wa Inca hawapo tena, lakini makabila madogo madogo

5. "Upendo Huamini Yote." Humtegemea kabisa Baba yetu wa mbinguni. Hufikiria mema kuhusu mwenzako.

6. "Upendo Hutumaini Yote." Upendo haushindwi. Humwezesha mtu kustahimili wakati wa shida.

7. "Upendo Hustahimili Yote." Upendo huendelea mbele hata wakati wa furaha na wakati wa shida. Upendo haupungui. Hutuwezesha kuwa na moyo wa "kuendelea na kazi" mpaka safari ifike mwisho. Upendo hauishi.

SEHEMU YA TATU: Yale Ambayo Upendo Hufanya

(Soma 1 Wakorintho 13:4-8) 1. Upendo hauna tamaa baya juu ya yale yanayotendwa na mtu mwingine. Na upendo haujifikirii. Upendo haujivuni.

2. "Upendo haujivuni na haukosi kuwa na adabu." Upendo hauna kiburi na haujipeleki mbele. Upendo hauna majivuno na kujiinua kama tausi.

3. "Upendo hautafuti mambo yake." Hautafuti upendeleo au faida au nafasi ya kuwashinda wale wengine. Upendo hujitoa wenyewe ili ndipo watu wale wengine wapate kuishi.

4. "Upendo hauoni uchungu na hauhesabu mabaya." Hauendi huku na huko kutafuta mabishano. Upendo haukasiriki. Hauna hasira na kuona uchungu upesi. Upendo hauhesabu mabaya uliotendewa.

5. "Upendo haufurahii udhalimu." Haufurahii maneno yanapoharibika au watu wengine wakikosa kufaulu.

Upendo haufurahii dhambi au tabia baya.

SEHEMU YA NNE: "Upendo Haupungui"

(Soma 1 Wakorintho 13:8-13).

Upendo haungamii. Upendo hauna mwisho. Upendo haupungui au kushindwa. Haushindwi katika kutimiza kusudi lake. Siku moja karama zile zingine za ajabu zitakoma zikimaliza kazi zake.

Ufahamu wetu na karama zetu zilizo nyingi ni haba sana. Sasa tunafikiria vile mtoto anavyofikiria. Ni kama kutazama ndani ya kioo; kila kitu hakionekani kuwa dhahiri. Lakini siku moja Mungu atafunua ufahamu wetu. Tutakuwa watimilifu ndani yake. Tutaona wazi kabisa. Kunayo mambo matatu ambayo yataidumu hata milele. Nayo mambo hayo ni imani, tumaini na upendo. Mambo hayo hayatakoma au kukosa kuwa na maana. Yataidumu hata milele. Lililo kuu ya hayo matatu ni upendo.

KIONGOZI:

Je, tunaweza kuonyesha kwa njia zipi jinsi tunavyompenda Kristo pamoja na watu wale wengine? Je, marafiki na jirani zetu huliona pendo la Kristo likipitia kwetu? Mara kwa mara tunawanung'unikia, kuwachukia, kuwaonea wivu, na kuwakasirikia watu wengine. Pendo la Kristo haliwezi kung'aa katika maisha yaliyojaa giza la makosa hayo. Tusipokuwa na upendo ushuhuda wetu wa Kikristo utakuwa bure. Ebu na tuyafungue maisha yetu yaingie pendo la Mungu katika Kristo ili yaweze kububujika kwa watu wengine, kwa maana Mungu ni pendo.

Mpango wa Pili

MCHUNGAJI MWEMA

Kilini cha Masomo: Maneno Makuu ya Biblia

Kifungu cha Kukumbuka:

"Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu."

Zaburi 23:1

Kuyasoma Maandiko: Zaburi 23

KIONGOZI

Ukiuliza mtu ye yote aseme ni Zaburi gani anayoipenda sana, pengine atajibu, "Zaburi ya 23." Roho Mtakatifu alimwongoza malme Daudi, ambaye hapo zamani alikuwa kijana mchungaji, kuandika habari za mchungaji wa milele mwenye upendo wa fadhili. Mchungaji huyu ambaye ndiye Bwana wetu, hutuongoza na kutulinda. Anaweza kuwa mchungaji kwa sababu aliyatoa maisha yake kwa ajili ya kondoo wake. "Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo" (Yohana 10:11). Upendo ule uliomfanya Bwana wetu kwenda mpaka Kalvari ni mkuu sana uwezao kuzitimiza haja zetu sasa. Ni upendo mkuu wa kuweza kutufikisha mbinguni.

SEHEMU YA KWANZA: "Bwana Ndiye Mchungaji Wangu, Sitapungukiwa na Kitu"

Daudi anatuambia ya kuwa yule aliyeumba ulimwengu ndiye mchungaji wake. Kila haja ya mwili, mawazo na roho hutolewa kutoka kwake Mungu. Mchungaji anazifahamu haja zetu na anazo nguvu za kutupatia riziki zetu.

Woga wa kupungukiwa huwafanya watu wengi kuanguka dhambini. Woga wa kukosa kuajiriwa kazi, woga wa kupata ajali, woga wa siku za usoni na mambo mengine mengi hutoweka tukijua ya kuwa Bwana ndiye mchungaji wetu. Kwa maana anatupenda hatutapungukiwa na mahali pa kupumzika wala kitu cha kunywa wala cha kula. Hatutakosa faraja wakati wa huzuni. Tutakuwa na ushindi wa kuwashinda maadui wetu, amani wakati wa shida, na furaha katika Bwana. Tutapata nguvu za kuhudumu na mahali pa makao baada ya safari ya hapa duniani. Je, amekosa kumpa mtu wake kitu cho chote ulimwengu anachohitaji? Mchungaji peke yake ndiye awezaye kutupatia vitu hivi. Jina lake lisifiwe!

SEHEMU YA PILI: "Malisho ya Majani Mabichi"

Mchungaji mwema, huwaongoza kondoo wake kwenye malisho mazuri na kuwalaza huko. Majani mabichi na maji ya utulivu hufariji mioyo yao. Pengine Daudi alifikiri habari za wakati ule alishindwa katika maisha kwa sababu ya dhambi alizozitenda na aibu aliyoiipata. Kwa muda wa mwaka mmoja Daudi alipatwa na shida, bila

amani ya mawazo na moyo mpaka siku ile alipozitazama dhambi zake, akalia kisha akazikiri na kuziungama kwa njia ya maombi mbele za mchungaji mwema aliyempenda. Baada ya kufanya hivyo mchungaji mwema akaifariji roho yake, akarudisha furaha ya wokovu wake, na akamfanya tena mfuasi afaaye kumfuata Bwana.

Je, roho yako iko vipi? Je, roho yangu iko vipi? Tunahitaji kuhuishwa? Je, unashindwa kwa sababu ya dhambi ambazo hujazikiri? Je! tunasikia kutokuwa na nguvu kwa sababu tunajiona kuwa tu peke yetu katika kumfuata Bwana? Ebu na tumwendee mchungaji mwema ili atuhishe kama vile apendavyo. Mchungaji mwema anataka kutupatia uhuisho huo sasa kwa njia ya upole na upendo.

SEHEMU YA TATU: "Sitaogopa Mabaya"

Baada ya maisha yetu kuhuishwa na kuongozwa, basi mchungaji mema hutuongoza katika njia za haki. Ingawa wakati mwingine njia hizi hupitia kwenye mashindano na kutokuwa na hakika, hupita katika uvuli wa mauti au sehemu za hatari, mwandishi wa Zaburi amesema ya kuwa, "Sitaogopa mabaya, kwa maana Wewe upo pamoja nami." Mchungaji anapowaongoza kondoo wake kupitia milima iliyo hatari kwenye malisho yenye mwangaza wa mwezi, kondoo huwa karibu na mchungaji. Hutii amri zake, huiisikia sauti yake, humtegemea mchungaji wao.

Daudi alifahamu ya kuwa alipopita kwenye hatari, huzuni, vita na kufa

moyo, mchungaji wake alikuwa karibu naye. Mchungaji wake huifahamu njia. Daudi alifahamu ya kuwa ikiwa Bwana ndiye kiongozi wake, hawezi kitu kingine cho chote. Mambo yote yangekuwa shwari.

SEHEMU YA NNE: "Moyo Wenye Upendo"

Daudi alimwona Bwana akiwa kama mtu anayemkaribisha mgeni wake kwenye meza yenye chakula kingi na kumpa mgeni wake mafuta yenye harufu nzuri. Yeye hamkaribishi mgeni wake faraghani mahali asijulikane na watu, bali humkaribisha mbele ya watesi wake. Bwana akiwa ndiye mwenye kukaribisha atatutunza na kutupa kila kitu tunachokihitaji, tena kwa wingi, kama kikombe kilichofurika maji.

SEHEMU YA TANO: "Siku Zote Za Maisha Yangu"

"Hakika wema na fadhili zitanifuata..., nami nitakaa nyumbani mwa Bwana milele," hivyo ndivyo Daudi mwandishi wa Zaburi alivyoandika. Licha ya Bwana kutupa haja zetu na kutuongoza, hata anatuongoza kutoka kwenye hatari ya adui zetu na hutuandalia meza ya ushirika wake. Kisha anatuahidi kuwa kunayo makao mwisho wa safari ya maisha haya na tumekaribishwa na huyo Mchungaji Mwema kukaa naye hata milele. Tutaishi naye milele katika makao yake.

KIONGOZI:

Je, ungependa kujua ndani ya moyo wako ya kwamba kunayo makao ambayo yametayarishwa kwa ajili

walianza kujitukuza na kujigamba. Washiriki ambao hawakuwa na karama hizi walianza kutamani na kuwa wagomvi. Paulo alitaka wafahamu kuwa ingawa vipawa vyao vilikuwa tofauti, vyote hutoka kwake Mungu. Alitaka marafiki zake wafahamu kuwa vipawa vyao havitakuwa na maana ikiwa pendo haliwezi kuandamana na kila kipawa. Vipawa vyetu vinapaswa kutekelezwa chini ya upendo. Sura ya 13 imelipatia kanisa la Korintho karama iliyo "bora zaidi," ni njia ya upendo (1 Wakorintho 12:31).

SEHEMU YA KWANZA: Kama Hatuna Upendo, Sisi si Kitu

(Soma 1 Wakorintho 13:1-3). Kama tungeandika orodha ya karama zote za kiroho zile ambazo tungependa kuwa nazo ili tumtumikie Mungu na wenzetu, orodha hiyo ingekuwa na mambo gani? Paulo ametuambia ya kuwa ikiwa pendo haliwezi kuonekana katika kila karama na kila huduma, basi mambo yote tunayojaribu kuyatenda yatakuwa bure.

1. Maneno au hotuba yo yote ya wanadamu au ya mbinguni, isipoandamana na upendo ni kama upatu uvumao.

2. Hata ikiwa ni ufahamu wa mpango wa Mungu wa kuwahudumu watu wake ni bure bila upendo.

3. Nijapojua siri zote na maarifa kama sina upendo "si kitu."

4. Nikiwa na imani ya kutenda mwujiza, na hata kipawa maalum cha roho, hakifai bila upendo.

5. Hata nikiwa na kazi ya kuwalisha wenye njaa na kuwapa maskini nguo, hata nikiutoa mwili wangu uungue moto au niuzwe kama mtumwa, bila upendo ni bure tu.

Upendo ndicho kitu kile kinachohitajika. Hakuna jambo linaloweza kutendeka bila upendo. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).

SEHEMU YA PILI: "Vile Upendo Unavyotenda"

1. "Upendo Huvumilia." Hufahamu mambo na kuyastahimili. Chini ya mateso, shida, majaribu na taabu upendo hauingizi jambo kwa nguvu na tena hautumii nguvu.

2. "Upendo hufadhili." Yesu alienda kila mahali akitenda mema. Aliutendea ulimwengu mambo mema na fadhili kuliko "vyema vyote vya starehe." Tunapaswa kuwa watu wenye huruma, na wenye kutunza. Pendo lile linalotoka kwa Mkristo linapaswa kuwa pendo la matendo, sio maneno tu, bali kwa matendo mema.

3. "Pendo hufurahi pamoja na kweli." Hufurahia ushindi wa maisha ya Mkristo ya kila siku. Hufurahia wakati watu wanachagua kutenda kweli.

4. "Upendo huvumilia yote." Upendo hufunika makosa, huwafanya watu kutunzana kila mtu na mwenzake. Upendo hautafunua wazi mashaka na makosa ya watu wengine.

Paulo hakuwa mtenda maajabu au mtu mwenye "nguvu nyingi za kiroho." Alimtegemea Kristo katika kila jambo. Paulo alifahamu ya kuwa bila Kristo hawezi kufanya lo lote (Yohana 15:5). Lakini katika Kristo aliweza mambo yote katika Yeye amtiaye nguvu (Wafilipi 4:13).

Mara kwa mara makanisa yetu yanawauliza washiriki wake wafundishe Shule ya Jumapili, kuongoza Ushirika wa Wanawake, kuongoza mikutano ya maombi, au kutumika katika sehemu zingine za kazi za kanisa. Wengine wetu tunakosea kwa kusema, "Siwezi kufanya," "Sijui jinsi ya kutenda," au "Ninaogopa." Tunayaweza mambo yote katika yeye atutiaye nguvu. Baraka zake Mungu hazikomi, zinazidi kuongezeka. Ghala lake linajaa na kufurika. Mungu wetu ni Mungu tajiri, yeye ndiye mwenye vitu vyote. Mungu hatuaibishi katika

Mpango wa Kumi

NJIA YA UPENDO

Kilini cha Masomo: Maneno Makuu ya Biblia

Kifungu cha Kukumbuka:

"Basi sasa inadumu imani, tumaini, upendo, na katika hayo lililo kuu ni upendo."
1 Wakorintho 13:13

Kuyasoma Maandiko: 1 Wakorintho 13

KIONGOZI:

Paulo aliliandikia kanisa la Korintho ili kulisaidia kushinda shida

kutukirimu na kila kitu tunachokihitaji.

Tukishirikiana naye Kristo kwa njia ya imani basi tutaunganishwa na asili ya utajiri wa kweli yote. Paulo amefunga barua yake kwa Wafilipi kwa kusema, "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu" (Wafilipi 4:19). Jina lake litukuzwe na lisifiwe!

KIONGOZI WA MPANGO:

Ebu tutumie muda wa dakika chache katika kutafakari. Tofauti kati ya moyo ulioshindwa na unao furaha, na kati ya kupungukiwa na kupata tele ni Kristo. Tofauti kati ya mateso na amani, na kati ya udhaifu na kuwa na nguvu, kati ya kutamani na kutosheka ni Kristo mwenyewe. Mungu alikuja akawa mtu, akawa maskini ili tuwe matajiri (2 Wakorintho 8:9).

iliyoingia katika ushirika wao. Katika sura ya 12, Paulo alilisaidia kanisa hili kuhusu karama za kiroho. Washiriki fulani waliopokea karama za kiroho

yako? Hayakubuniwa na mikono ya watu, bali ni mji wa milele kule mbinguni. Mji huo unaweza kuwa wako ikiwa umemkubali mchungaji mwema kuwa Mwokozi wako. Mwana

wa Mungu aliyatoa maisha yake pale Kalvari kwa ajili yetu. Mwaamini Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi na mchungaji wako.

Mpango wa Tatu

MTUMISHI MWENYE HUZUNI

Kilini cha Masomo: Maneno Makuu ya Biblia

Kifungu cha Kukumbuka:

"Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote."
Isaya 53:6

Kuyasoma Maandiko: Isaya 53

KIONGOZI

Kitabu cha Isaya 53 ni kama "Habari Njema" katika Agano la Kale. Huonyesha ya kuwa mshahara wa dhambi ni mauti. Sura hii inaeleza kuwa Yesu Kristo alilipa deni ya makosa yetu kwa njia ya kuteswa akafa mahali petu na kwa ajili yetu. Hutuambia ya kuwa tunapatanishwa na Mungu ikiwa tutampokea Yesu Kristo kuwa Mwokozi wetu. Na hutuambia habari za ushindi ule tuwezao kuwa nao juu ya dhambi ikiwa tunamwamini Yesu Kristo aliyе Mwana wa Mungu. Kitabu cha Isaya kiliandikwa miaka mia kadha iliyopita kabla Yesu Kristo hajazaliwa. Nabii alikuwa na hakika kwamba Kristo ndiye sadaka ya kutosha hata akaandika kitabu cha Isaya 53 kana kwamba jambo hili lilikuwa limekwisha tukia.

SEHEMU YA KWANZA: "Maisha ya Mtumishi" (Isaya 53:1-3)

Watu wa zamani za nabii Isaya walifikiria kwamba yule ambaye atakuwa mkombozi atawaangamiza maadui zao. Kisha walifikiri, atasimamisha ufalme wake imara hapa duniani. Hawakuweza kuamini taarifa ile iliyosema ya kuwa huyo mtumishi atazaliwa na bikira na kukua bila watu kumfahamu. Huyu mtumishi alipokua akawa mtu mzima hakuwa na kitu kisicho cha kawaida ambacho kiliweza kuwavuta watu wake. Hakuwa na "duara ya mwangaza" iliyomzunguka kichwani mwake. Hakuvaa mavazi ya askari au shujaa; hakuwa kiongozi wa serikali. Yesu Kristo alipowaambia watu ya kuwa yeye ndiye aliyekuwa Masihi aliyeahidiwa, ambaye ufalme wake siyo wa ulimwengu huu, watu walimkataa. Wakamchukia,

wakamwacha na hata wakamsulibisha msalabani.

SEHEMU YA PILI: "Mateso ya Mtumishi Huyo" (Isaya 53:4-6)

Wakati mtumishi huyo mwenye kuteswa alipouawa, watu walikiri ya kwamba alizitwaa dhambi za wenye dhambi. Ikiwa utalibadilisha neno linalotajwa kwa wingi ("yetu" au "sisi") kuwa neno la mtu mmoja ("yangu" au "mimi") kisha utumie jina "Kristo" mahali pa "Yeye" utakuwa na ufahamu zaidi:

Kif. 4. Hakika Kristo ameyachukua masikitiko yangu, amejitwika huzuni zangu.

Kif. 5. Bali Kristo alijeruhiwa kwa makosa yangu, na alichubuliwa kwa maovu yangu na kwa kupigwa kwake Kristo, mimi nimepona.

Kif. 6. Mimi kama kondoo nimepotea, nimegeukia njia yangu mwenyewe na Bwana ameweka juu ya Kristo maovu yangu yote.

SEHEMU YA TATU: "Kifo cha Huyo Mtumishi" (Isaya 53:7-9)

Huyo mtumishi aliteswa vibaya sana. Alinyenyekea katika mateso yake lakini hakufunua kinywa chake. Kwa nini alikaa kimya wakati wa mateso yake? Kwa sababu alijua kusudi la Mungu; alifahamu kuwa aliteswa kwa sababu ya watu wengine. Huyo mtumishi alihukumiwa kufa. Hakuna mmoja aliyefahamu kuwa kifo chake kilikuwa kwa sababu ya dhambi zao. Hata wakati wa kufa kwake kutendwa jeuri kuliendelea na hata chuki haikukoma pale kaburini.

Hakuwa na hatia wala dhambi, na alikuwa Mwana aliyependewa na Babaye. Yesu Kristo alisema, "Hakuna mtu aniondoleaye, bali mimi nautoa mwenyewe" (Yohana 10:18).

SEHEMU YA NNE: "Mshindi wa Huyo Mtumishi" (Isaya 53:7-9)

"Lakini Bwana aliridhika kumchubua" (Isaya 53:10). Mungu hakufurahia kuteswa kwa huyo mtumishi; lakini aliyastahimili mateso yake ili mapenzi yake yatendeke ili wokovu upatikane. Mtumishi wa Mungu aliye mtakatifu akawa dhabihu ya dhambi ya watu wote. Kifo chake kilikuwa mpango wa Mungu wa ukombozi. Kifo chake kilileta wokovu kwa watu wote. Mtumishi huyo wa milele, aliyeteswa, na kukataliwa, akauawa. Alifufuka na sasa anaishi na kuwaombea wenye dhambi. Yesu alimshinda Shetani, dhambi na kifo. Huwapa ushindi wale wote wanaomwamini.

KIONGOZI WA MPANGO:

"Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba" (Wafilipi 2:5-8).

Mchezo: Katika Agano Jipya kuna vifungu vingi ambavyo ni sawa na

Kristo. "Furahini katika Bwana sikuzote; tena nasema, furahini."

SEHEMU YA PILI: "Na Amani ya Mungu"

(Soma Wafilipi 4:6-7).

Paulo ametufundisha ya kuwa jawabu la shida na huzuni zetu ni kuamini katika maombi. Peleka woga wako, shida zako na huzuni zako kwake Bwana, kwa njia ya maombi "pamoja na kushuruku." Paulo ametushauri tuombe kwa shukrani bila kujitaabisha. Usijali kwamba itamchukua Mungu muda gani kuyajibu yale yote uliyomwomba. Lakini unaweza kumshukuru kwa sababu ya kukubaliwa kukikaribia kiti cha Mungu cha enzi.

"Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu". Kusihi maisha ya kuyategemea maombi kutaisaidia mioyo na akili zetu na hutusaidia kumtumainia Mungu. Namna ya amani ya Mungu hupita ufahamu wetu. Amani yake ni kama askari anayelinda mlango wa maisha yetu, akiulinda ili kitu kiovu kisiingie na kuharibu imani na kuondoa amani ya roho na akili tuliyo nayo katika Yesu Kristo.

SEHEMU YA TATU: "Yatafakarini Hayo"

(Soma Wafilipi 4:8-9).

Mawazo yetu yanaweza kutonyang'anya amani ya moyo na ya nia zetu tunazozipata kutoka kwa Yesu. Kama tukiendelea kufikiri habari za makosa na kushindwa

ambako tulikiri na kusamehewa na Baba Yetu wa mbinguni, basi amani yetu itatoweka. Ikiwa wazo la tamaa mbaya litaingia ndani ya nia zetu, kisha linaendelea kukaa pale ndani, basi amani yetu haitaendelea kudumu. Ikiwa mtu mmoja atatukosea kisha tuanze kuwaeleza jambo watu wengine na kuyaweka mambo hayo ndani ya moyo, chuki yetu itafukuza amani yetu.

Paulo aliwaambia watu wa Filipi wayatafakari yaliyo ya kweli, staha, haki, safi na yote yaliyo yenye sifa njema, wema wo wote na hata sifa nzuri. Tunapaswa kuyafikiria mambo yale ya kumtukua Mungu. Wafilipi walikuwa wamekwisha mwona Paulo akifanya kazi na kuhudumu. Walimwona akifikiri na kufundisha. Walijua ya kuwa alikuwa akitawaliwa na roho wa Kristo. Paulo alikuwa na haki ya kuwaambia wao na hata sisi, "Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi" (Wafilipi 4:9). Paulo alikuwa kielelezo kikubwa kwa maana alikuwa mtu aliyezoea amani na kutosheka hata kukiwa na shida gani kwa sababu maisha yake yalisimama katika Yesu Kristo.

SEHEMU YA NNE: "Nayaweza Mambo Yote Katika Kristo"

(Soma Wafilipi 4:12-13, 19). Paulo alifahamu kuwa anayaweza mambo yote ya hali yote katika Kristo anayempa nguvu. Ingawa Paulo alikuwa mtu mwenye elimu, hakutegemea elimu yake mwenyewe.

Mpango wa Tisa

AMANI YA MUNGU

Kilini cha Masomo: Maneno Makuu ya Biblia

Kifungu cha Kukumbuka:

"Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu." Wafilipi 4:19

Kuyasoma Maandiko: Wafilipi 4:4-9, 12-13, 19-20

KIONGOZI:

Wakati Paulo alipoandika kitabu cha Wafilipi alikuwa mfungwa wa serikali ya Kirumi. Waraka huu uliandikiwa kanisa alilolipenda sana la Filipi. Paulo aliteswa sana kwa sababu ya kuhubiri Injili ya Yesu Kristo. Alikumbwa na watu wenye ghasia, alipigwa mawe, na mara nyingi alifungwa gereza. Siku moja alipokuwa kule Yerusalemu akizikusanya sadaka za kuwasaidia Wakristo maskini, alikumbwa na umati wa watu na angaliweza kuuawa kama afisa wa Kirumi hangalimwoko na kumweka gereza. Alipokuwa akisafirishwa kutoka gereza la Yerusalemu kwenda mpaka Roma, meli aliyosafiria ilivunjika kwa sababu ya dhoruba. Wakati alipokuwa akiwaandikia Wafilipi, Paulo alikuwa akingoja kwa muda wa miaka miwili ili apelekwe mahakamani. Alifungwa na mnyororo kwa askari wa Kirumi. Lakini hata hivyo barua yake imejaa pendo na faraja.

SEHEMU YA KWANZA: "Furahini Katika Bwana Sikuzote"

(Soma Wafilipi 4:4-8). Je, ni kitu

gani kilichomfanya Paulo kusema kuwa, "Furahini katika Bwana?" Yeye alikuwa maskini. Aliacha kila kitu ili ndipo amfuate Kristo, utajiri wake, kazi yake kama afisa wa kuhani mkuu, haki za uraia wake hata starehe za kwao nyumbani. Kila kitu alichokuwa nacho alikihesabu kuwa kama takataka ikilinganishwa na faida ya kumjua Yesu Kristo (Wafilipi 3:7-9). Paulo alikuwa mgonjwa sana hata alikuwa nusu la kufa. Meli yake ilivunjika. Alikuwa mfungwa aliyefunganishwa na askari wa Kirumi. Lakini tunamwona akifurahi na kushukuru kwa maana kuwa ndani ya gereza kulimpatia nafasi ya kutangaza Injili, na hasa katika kuwafikia askari wa kifalme. Alifurahi kwa sababu Wakristo wengine walipata shauku ya kuwa na ujasiri wa kunena Neno la Mungu.

Je, siri na furaha na amani za Paulo zilikuwa nini? Paulo alikuwa mtu mwenye maono. Maoni yake yalimpelekea mpaka Korintho, Efeso, Kolosai, Filipi na katika miji na vijiji akihubiri injili yake Kristo. Na sasa, ingawa yumo gereza anauona ulimwengu wote ukiwa mali Yake

vifungu vya Isaya. Gawa washiriki wanaohudhuria katika makundi mawili. Watu wa kundi moja wasome maandiko ya nabii Isaya inayoandikwa chini upande wa kushoto. Watu wa kundi lile lingine wasome vifungu vya Agano Jipya vinavyoandikwa chini upande wa kulia.

1. Isaya 53:12

Luka 22:37

2. Isaya 53:8

Matendo 8:33

3. Isaya 53:5

Warumi 4:25

4. Isaya 53:1

Warumi 10:16

5. Isaya 53:15

Warumi 15:21

6. Isaya 53:9

1 Petro 2:22

7. Isaya 53:7

1 Petro 2:23

8. Isaya 53:5

1 Petro 2:24

9. Isaya 53:6

1 Petro 2:25

10. Isaya 53:4

Mathayo 8:17

11. Isaya 53:1

Yohana 12:28

Mpango wa Nne

BABA MWENYE PENDO

Kilini cha Masomo: Maneno Makuu ya Biblia

Kifungu cha Kukumbuka:

"Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako." Luka 15:18

Kuyasoma Maandiko: Luka 15:11-32

KIONGOZI

Mara kwa mara Yesu alitumia mifano ya maneno alipotaka kusimulia habari za ufalme wa mbinguni. Hadithi ya "Mwana Mpotevu" ni mfano wa maneno unaoeleza habari za pendo la Mungu. Mungu hapumziki mpaka afanye jambo la kuwaonya wapotevu, kuwatafuta watu waliopotea, na kuwapata wale walipotea na kuwarudisha kwake kwa njia ya Yesu Kristo.

SEHEMU YA KWANZA: Mji Mzuri

Baba mmoja alikuwa na wana wawili. Waliishi pamoja katika nyumba yao nzuri na walikuwa na chakula kingi. Yule mwana mdogo alichoka na hali ya kukaa kwao nyumbani na alitaka kuwa huru kutoka katika mamlaka ya babaye. Alimwambia baba yake ampe urithi wake ili ndipo aende zake. Mali ya baba yangaligawiwa hao wana wawili baada ya babaye kufa. Pengine babaye

alitaka huyo mwana akae karibu naye. Pengine alikuwa na huzuni nyingi kwa kutambua shida ile ambayo itampata mwanaye. Lakini baba hakupenda mwanaye ayafuate mapenzi yake kwa lazima. Naye alimpa huyo mwana sehemu ambayo ingalimwangukia.

SEHEMU YA PILI: Kwenda Nchi ya Mbali

Naye huyo mwana alienda mbali kutoka kwa babaye. Sasa aliweza kuishi kama alivyopenda. Katika nchi hiyo ya mbali, hapakuwa na mtu hata mmoja aliyemwambia kwamba yale ambayo alikuwa akifanya yalikuwa makosa. Hajapata kuwa na pesa nyingi na marafiki wengi kama hao hapo mbeleni. Hatimaye pesa zake zilikwisha nao marafiki wake wote walimtoroka. Kulitokea njaa kubwa katika nchi hiyo. Mara yule mwana alianza kuhitaji sana hata alienda kutafuta kazi ya kuwalisha nguruwe. Wayahudi walifikiria kuwa nguruwe walikuwa wanyama wachafu na kwa hiyo hawakupenda kufanya jambo lo lote kuhusiana na nguruwe. Hata hivyo yule mwana aliona njaa sana hata alianza kujishibisha na maganda yale ambayo nguruwe walikuwa wakijishibisha nayo.

SEHEMU YA TATU: Mwana Mwenye Toba

Yule mwana mdogo alipokuwa akiwalisha wale nguruwe alianza kuzingatia moyoni mwake vile mambo yalivyokuwa mazuri kwa nyumbani. Alikuwa na baba aliyependa. Kulikuwa na chakula kingi na hata watumishi wa kumsaidia. Alifahamu ya kuwa ingefaa sana kama angekuwa

mtumishi wa babaye kuliko kufa na njaa alipowalisha nguruwe. Naye alitambua ya kuwa alikuwa amekwisha tenda dhambi mbele za babaye na mbinguni. Alikata shauri kurudi nyumbani na kuomba msamaha. Aliomba afanywe mtumishi wa kufanya kazi ya kila siku.

SEHEMU YA NNE: Baba Mwenye Upendo

Yule kijana alipokuwa akitembea kurudi nyumbani, alikuwa akifikiria vile babaye atamwambia. Moyo wake ulikuwa na aibu nyingi. Hafai kuitwa mwana tena. Atamwomba babaye kumfanya kuwa mtumishi. Yule kijana alipokuwa akiondoka nyumbani alikuwa akimwambia baba "Nipe." Sasa anamwambia "Nifanye." Lakini yule mwana hakuwa na nafasi ya kuomba msamaha afanywe kuwa mtumishi. Baba mwenye upendo alikuwa akimtarajia kila wakati. Baba alikimbia na kumkaribisha kurudi nyumbani kwa mikono miwili. Baba aliagiza avikwe vazi lililo bora na atiwe viatu miguuni. Wakamchinja ndama wakala wakafurahi. Akaweka pete ya jamaa katika kidole chake akisema, "Kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa; naye amefufuka, alikuwa amepotea, naye ameonekana." (Luka 15:24). Roho ya babaye ilikuwa na furaha nyingi. Naye Mungu yuko vivyo. Yeye husamehe na kurudisha ushirika uliovunjika kwa kila mtu anayerudi kwake.

SEHEMU YA TANO: Mwana Yule Mkubwa

Yule mwana mkubwa alirudi kutoka katika shamba la babaye.

kukaa pamoja naye. "Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi" (Zaburi 103:12).

Basi ni nani tena awezaye kutuhukumu? Yesu peke yake ndiye mwenye haki ya kutuhukumu. Bali hatutahukumiwa naye kwa maana ni yeye mwenyewe aliyetufia na halafu alifufuka. Sasa anakaa mahali pa heshima karibu na Mungu akituomba huko mbinguni.

SEHEMU YA NNE: Hatuwezi Kutenganishwa na Upendo wa Kristo

(Soma Warumi 8:35-39).

Paulo anauliza swali, "Ni nani atakayetutenganisha na upendo wa Kristo?" (Warumi 8:35). Halafu anaendelea kutaja orodha ya hayo majaribu, na mengi ya hayo alikuwa amepitia ndani yake: dhiki, shida, adha, njaa, uchi, hatari au upanga. Mambo hayo hayawezi kututenganisha na pendo la Kristo. Shida hizo zinaweza kututenganisha na mali, au afya, au jamaa zetu, au marafiki zetu au faraja au starehe. Lakini mambo hayo hayawezi kushinda pendo la Kristo ambalo halibadiliki.

Kwa kuyataja maneno ya Zaburi 44:22, Paulo anasema ya kuwa majaribu ni kama mateso

yanayoendelea na kuzidi. Inaonekana kama tunauawa mchana kutwa, na tunafanyiwa kuwa kama kondoo waendao kuchinjwa. Lakini mateso kama hayo hayaonyeshi ya kuwa pendo la Mungu limebadilika au kunalo jambo ambalo limetutenganisha na pendo hilo. Tunapoendelea kuishi katika pendo lake, tutakuwa zaidi ya washindi.

Maisha au mauti haziwezi kututenganisha na pendo lake Kristo. Tunaishi maisha pamoja na Kristo; tukifa tunakufa pamoja naye; na tukifa pamoja naye tutafufuka naye pia. Kifo ni hatua ya kutufikisha kuwa pamoja na Kristo. Hakuna kitu kilichoombwa, au kiumbe, au uwezo wo wote uwezao kututenganisha na pendo la Mungu katika Kristo Yesu, Bwana wetu.

KIONGOZI:

Pendo lake Mungu ni la milele. Linadumu na halibadiliki. Ni la kutosha na linashinda. Mungu akiwa ndani ya Kristo hutupenda hata kukitokea kitu cho chote katika maisha yetu. Pendo lake hufanya kazi katika hali yo yote ili mambo yote yanayotukia kwetu yafanye kazi pamoja kwa kusudi njema linalolingana na mpango wake. Sisi ni zaidi ya washindi katika Kristo aliyetupenda.

tufanane na Kristo. Hakuna mtu au kitu kiwezacho kututenganisha na pendo la Mungu katika Kristo.

SEHEMU YA KWANZA: Kusudi la Mungu

(Soma Warumi 8:28-30).

Mtume Paulo anasema ya kuwa, "Twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani wale walioitwa kwa kusudi lake" (Warumi 8:28). Mungu mwenye huruma na mkarimu huvitawala viumbe vyote. Anaweza kubadilisha ugonjwa, taabu, shida, mateso na huzuni kuwa baraka kwa wale wanaoendelea kumpenda, kwa wale wanaotaka kusudi lake litendeke katika maisha yao. Tunaweza kutumainia kuwa yale yote yanayotukia mwishowe yatakuwa faida yetu. Ni lazima tumtegemee huyo Mungu mwenye upendo; ni lazima tuishi katika imani. Ukweli huu ni lazima utuinue juu zaidi tushinde wasiwasi, manung'uniko, woga na mashaka.

Mungu alituchagua ili atupatie wokovu wake kabla ya ulimwengu huu kuumbwa (Warumi 8:29). Kusudi lake lilikuwa kwamba kila siku tuzidi kufanana na Yesu Kristo. Mkristo akizidi kufikiria wokovu huu, hutambua ya kuwa haukufika kutoka yeye mwenyewe; ulitoka kwake Mungu. Yesu alikuja hapa duniani, akaishi, akafa msalabani, na mwishowe alifuka tena. Mkristo hakufanya cho chote kuleta wokovu wake; ilikuwa kazi yake Mungu peke yake. Tumekwisha sikia habari za

pendo hili la ajabu. Sisi sio tuliotunga hadithi hiyo; tulipokea habari zake.

SEHEMU YA PILI: Mungu Yu Pamoja Nasi

(Soma Warumi 8:31-32).

"Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?" (Warumi 8:31). Ikiwa Mungu yu pamoja nasi, haidhuru ni nani atakayetupinga. Hakuna nguvu zilizopo mahali po pote zinazoweza kushinda nguvu za Mungu. Ulimwengu, mambo ya kimwili na hata Ibilisi anaweza kutupinga, lakini hayo yote hayawezi kushinda ikiwa Mungu yupo upande wetu.

Ukweli ulio wazi ni kwamba Mungu anatupenda na yupo upande wetu. Hakutunyima mwanaye bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote. Mungu alizidi kutonyesha pendo lake zaidi, "atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?" (Warumi 8:32). Ikiwa Mungu alitupa Mwanaye afe msalabani kwa ajili ya wenye dhambi, atazidi kutupatia vipawa vya kutusaidia na kutufanya kuwa kama Kristo.

SEHEMU YA TATU: Tumeishafanywa Kuwa Wenye Haki

(Soma Warumi 8:33-34).

Mkristo amepatanishwa na Mungu kwa sababu ya kumwamini Yesu Kristo. Amekwisha pata msamaha wa dhambi. Mungu ambaye ndiye hakimu, ametufanya kutokuwa na hatia. Ni nani awezaye kutuhukumu? Mungu ametuchagua kuwa watu wake. Mungu ametusamehe akatupa haki ya

Alisikia sauti ya nyimbo na machezo ya kumkaribisha huyo mgeni. Alisikia ya kuwa ndugu yake amerudi na karamu ilitayarishwa kwa ajili yake. Baba yake alikuwa na furaha! Nduguye mdogo alikuwa na furaha! Nyumba yote ilikuwa na furaha. Husuda, wivu na kujifikiria ziliujaa moyo wa huyo ndugu mkubwa hata alikataa kuingia ndani ya nyumba. Baba alitoka nje akamsihi huyo mwana mkubwa aingie ndani ya nyumba ili wafurahi. Lakini huyo mwana mkubwa alikataa. Hakufurahi kwamba ndugu yake amerudi nyumbani. Yule mwana aliteta akisema kwamba hajafanyiwa cho chote ingawa alizishika amri za babaye. Baba alimkumbusha yule mwana habari za urithi atakaokuwa nao. Naye akamkumbusha huyo ndugu mkubwa habari za uhusiano wa kijamaa kati yake na huyo ndugu mdogo kwa kubadilisha "huyu mwana wako" kuwa "huyu ndugu yako" (Luka 15:30, 32). Hadithi inamalizika kwa

kusema kuwa huyo mwana mkubwa alikataa kuingia ndani ya nyumba ya babaye kwa sababu ya kukataa kushiriki pendo la babaye.

KIONGOZI

Mungu amefanana na huyo baba mwenye upendo aliyeko katika hadithi hii. Mungu anapenda kusamehe na kutoa. Malaika wa mbinguni hufurahia wokovu wa mwenye dhambi. Mungu huwapenda wenye kuasi kama alivyompenda huyo mwana mdogo. Pia huwapenda wale wanaojifanya kuwa watakatifu na wasio na upendo kama huyo mwana mkubwa.

Ebu na tujiulize swali hili: Je, tunafurahi tunapowaona watu "wapotevu" wakiingia katika jamii ya Mungu? Pendo lake Mungu ni kwa ajili ya watu wote. Ebu na tumwombe Mungu atuongoze kwenda kwa waliopotea na atusaidie kuwa na sehemu yetu ya kuwaelekeza njia ya kwenda nyumbani.

Mpango wa Tano

NJIA YENYE FURAHA

Kiini cha Masomo: Maneno Makuu ya Biblia

Kifungu cha Kukumbuka:

"Heri walio maskini wa roho; maana ufalme wa mbinguni ni wao." Mathayo 5:3

Kuyasoma Maandiko: Mathayo 5:1-12

KIONGOZI

Katika "Hotuba Yake Mlimani" Yesu alifundisha ya kuwa Wakristo

wanaweza kuifahamu furaha na kweli. Furaha hii haitegemei kile uwezacho kufanya au kile uwezacho kutimiza,

lakini hutegemea walio maskini wa roho, wenye huzuni, wenye upole, wenye njaa na kiu ya haki, wenye rehema, wenye moyo safi, wenye kupatanisha na wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki, hao ndio wenye furaha katika ufalme wake Kristo.

SEHEMU YA KWANZA: Walio Maskini wa Roho na Wenye Huzuni

(Soma Mathayo 5:3-4). Watu wengi waliomsikiliza Yesu walikuwa watu maskini. Lakini Yesu aliwafundisha ya kuwa wenye furaha ni wale wanaofahamu unyonge wa hali yao ya kiroho. Wanafahamu kuwa wao ni maskini wa kiroho na wanamtegemea Mungu atakayewapa na kuwatimizia haja zao. Naye Mungu atawapa ufalme wa mbinguni.

Furaha huwa kwa wale wenye huzuni kwa sababu ya dhambi zao. Watu kama hao watafarijiwa na kupewa nguvu za kushinda dhambi. "Moyo uliovunjika na kupondeka, ee Mungu, hutaudharau" (Zaburi 51:17).

SEHEMU YA PILI: Walio Wapole na Wenye Njaa na Kiu ya Haki

(Soma Mathayo 5:5-6).

Wapole ni wale wanaopokea ufalme wake Yesu aliye mfalme. Ni wale ambao huzipenda amri za ufalme Wake. Maana yake upole ni kusema kutokuwa mkali, kumfikiria mwenzako, na kuwa mwenye fadhili. Wenye upole hawainyakui "nchi bali wanairithi." Heri ni wale wenye njaa na kiu ya haki mbele zake Mungu. Mara kwa mara tunatafuta kile tunachotamani sisi wenyewe. Ikiwa tutakuwa na "shauku ya haki, na

kupenda mambo ya kiroho, Mungu atatupa shauku zaidi ndani ya mioyo yetu. Tutatosheleka kabisa.

SEHEMU YA TATU: Heri Wenye Rehema na Moyo Safi

(Soma Mathayo 5:7-8).

Mwenye rehema hufurahi kwa kukumbuka rehema ya Mungu aliyotoa msalabani pale Kalvari. Anafahamu furaha iletwayo na hali ya kusamehewa. Mwenye rehema huwasamehe wale wengine. Msamaria Mwema ni kielelezo cha mtu mwenye rehema. Ingawa Wasamaria walionewa na Wayahudi, Msamaria Mwema alisimama safarini mwake ili amtunze yule Myahudi aliyepigwa na wevi.

Heri wenye moyo safi mbele zake Mungu. Moyo safi huyafanya maisha kuwa safi. Hatuwezi kwenda mbele za Mungu aliye mtakatifu ikiwa mioyo yetu siyo safi. Ikiwa tutamwona Mungu ni lazima mawazo, maongeo na maisha yetu yawe safi.

SEHEMU YA NNE: Heri Wapatanishi na Wenye Kudhuriwa kwa Ajili ya Haki

(Soma Mathayo 5:9-10).

Wapatanishi huitwa watoto wa Mungu kwa sababu yale wanayofanya ni yale yaliyofanywa na Mungu. Mungu ndiye mpatanishi mwema zaidi. Tangu mtu wa kwanza alipotenda dhambi, Mungu hujaribu kujipatanisha na mtu huyo. Wapatanishi hupenda kuwapatanisha watu wa Mungu na hupendana wao kwa wao.

mwanadamu. Alijua maana ya kujaribiwa, kuona njaa, na kuchoka. Alijua kutawaliwa na watu na kuteswa. Maneno ya Yesu yalikuwa maneno ya Mungu yaliyozungumzwa na watu. Matendo yake yalikuwa nguvu zake Mungu zilizomiminika kumpita yeye zikiwafikia watu. Yesu aliwaambia wanafunzi wake wamwamini.

SEHEMU YA NNE: "Mkiomba Lo Lote"

(Soma Yohana 14:12-14).

Yesu aliwaahidi wanafunzi wake mambo mawili makuu. Aliwaambia ya kuwa siku moja wao wataweza kufanya yale ambayo yeye hufanya, na hata watatenda zaidi. Maana ya Kristo kuwa ndani yetu ni kuwa tunaweza kudai nguvu zake Mungu kama vile Yesu alivyofanya. Sababu moja inayotuzuia tusitumiwe na Mungu kwa njia kuu ni kwa sababu ya

kutomwamini na kutomtegemea Kristo.

Ahadi ya pili ni kwamba ombi lo lote, litakaloombwa katika jina la Yesu na ambalo litamtukuzisha Baba katika Mwana, litajibiwa. Hakuna mpaka wa kitu cho chote tutakachokiomba kwa maana tumeambiwa kuomba "lo lote." Kusudi letu katika kuomba ni lazima liwe la kuleta utukufu kwake Mungu. Kwa maana tunajua kuwa Yesu Kristo yu nani, tunaomba katika jina la Yesu, tukiamini kwamba mapenzi yake yatatendeka.

KIONGOZI:

Tunaishi katika nyakati zenye shida. Mara kwa mara mioyo inafadhaika. Ebu na tukumbuke ya kuwa Yesu Kristo ndiye njia, kweli na uzima. Yeye ni kila kitu. Anataka kuishi ndani yetu na kutufanya kuwa Wakristo wenye kufaulu ambao maisha yao tatamtukuzisha Baba.

Mpango wa Nane

ZAIDI YA WASHINDI

Kilini cha Masomo: Maneno Makuu ya Biblia

Kifungu cha Kukumbuka:

"Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda kwa yeye aliyetupenda."

Warumi 8:37

Kuyasoma Maandiko: Warumi 8:28-30

KIONGOZI WA MPANGO

Warumi sura ya 8 inazo kweli nyingi za ajabu ambazo huweza

kuifanya mioyo yetu imsifu. Kifungu cha mwisho cha sura hii kuu kinatukumbusha ya kuwa Mungu huutawala ulimwengu, akitufanya

aliwafundisha wanafunzi ya kwamba wakati wa siku za shida ni kitu kimoja cha kufanya tu, kumwamini Mungu na kumwamini Yeye kama Mwokozi wao.

SEHEMU YA KWANZA:
"Mnamwamini Mungu, Niaminini na Mimi"

(Soma Yohana 14:1). Mara nyingi Yesu aliongea habari za kifo chake. Lakini sasa kifo chake kilikuwa kimekaribia sana. Alitaka kuhakikisha kwamba wanafunzi wake walikuwa tayari. Hakutaka wafadhaike moyoni. Yesu aliwaomba wanafunzi wake wamwamini yeye kama walivyomwamini Mungu, kwa sababu kama wangepanya hivyo ingelea faraja na ujasiri wakati wa kifo chake. Tunaweza kumwamini Yesu na kutegemea hekima yake, kazi yake, Neno lake na kutarajia kurudi kwake. Yesu ndiye thibitisho kwamba Mungu anataka kutupa sisi kila kitu anacho cha kutoa.

SEHEMU YA PILI: "Nitakuja Tena"

(Soma Yohana 14:2-4).

Wanafunzi walifadhaika sana Yesu alipowaambia ya kwamba ataenda zake (Yohana 13:31-38). Walitaka kujua kule ambako Yesu atakwenda. Naye Yesu aliwaambia ya kuwa ataondoka hapa ulimwenguni kwenda mbinguni kwa Babaye. Alisema, "Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi" (Yohana 14:2). Hii ni kusema ya kuwa mbinguni mna makao kwa ajili ya kila mtu. Yesu aliwaambia kwamba anawatangulia ili kuwaandalia mahali na wakienda watakaa pamoja naye.

"Nikienda...nitakuja tena." Yesu yuaja tena! Kama vile alivyokuja hapa duniani mara ya kwanza wakati malaika walipoimba, "Atukuzwe Mungu juu mbinguni," ndivyo atakavyorudi tena. Mara ya kwanza alikuja mtoto Mwokozi. Mara ya pili atakuja kama mfalme wa kuwatawala wafalme wale wengine. (1 Wathesalonike 4:16 na Mathayo 25:31).

SEHEMU YA TATU: "Njia, Kweli na Uzima"

(Soma Yohana 14:4-11).

Tomaso alikiri akisema ya kuwa hakujua mahali ambapo Yesu atakwenda wala hakuijua njia. Yesu alijibu, "Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6). Wayahudi walifahamu ya kwamba walipaswa kutembea katika njia "zake Mungu" (Zaburi 27:11). Walitaka kuchagua kweli (Zaburi 119:30). Walitaka kuishi maisha yale yafaayo kuishi. Yesu ndiye njia peke yake ya kufika kwake Baba. Yesu ndiye njia ya kufika nyumbani kwa Baba yake. Yesu ndiye kweli kuhusu Mungu ambaye huwafanya watu kuwa huru (Yohana 8:32). Yesu ndiye uzima wa Babaye (Yohana 6:32-35).

Naye Filipo alimwambia Yesu awaonyeshe huyo Baba. "Aliyeniona mimi amemwona Baba," Yesu alijibu (Yohana 14:9). Ukimwona Yesu umekwisha mwona Mungu. Mungu aliingia katika mfano wa mwanadamu katika Yesu Kristo akaja hapa duniani akiwa kwa hali ya mwanadamu. Hakuona haya ya kufanya kazi kama

Heri ni wale wanastahimili kuudhiwa kwa sababu yake Kristo na kwa ajili ya haki. Watu wasiomjua Mungu hawataki nuru yake iwaangazie. Hawataki haki yake ije ikabadilishe desturi, utamaduni, biashara au tabia zao. Yesu aliwaahidia ufalme wa mbinguni wale ambao wataudhiwa kwa sababu ya kuueneza ufalme wake hapa duniani.

SEHEMU YA TANO: Heri kwa Kushtumiwa kwa Uongo kwa Ajili Yangu

(Soma Mathayo 5:11-12).

Heri ni wale wanaofurahi wakishutumiwa na kuteswa na kunenewa maneno ya uongo kwa sababu wao ni wafuasi wa Yesu Kristo. Ikiwa tutaudhiwa kwa sababu yake Kristo, basi tutahesabiwa pamoja na manabii wa hapo kale, nao mitume "walifurahi kwa sababu wamehesabiwa

kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya jina hilo" (Matendo 5:41). Wakristo wa hapo mwanzo walisema, "Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi" (2 Wakorintho 4:8-9).

KIONGOZI

Kumfuata Kristo kila siku huleta thawabu. Wale walio wapole huirithi Ufalme wa Mbinguni. Wale wanao huzuni hupata faraja. Wenye njaa hujazwa. Wenye rehema hupata rehema. Heri wenye haki kwa maana watamwona Mungu. Wale wanaoteswa hupokea thawabu ya mbinguni.

Wale ambao ni sehemu ya ufalme wa Mungu huwa na furaha hapa duniani na wanatazamia furaha zaidi katika ulimwengu ujao.

Mpango wa Sita

JINSI YA KUOMBA

Kiini cha Masomo: Maneno Makuu ya Biblia

Kifungu cha Kukumbuka:

"Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe."

Mathayo 6:9

Kuyasoma Maandiko: Mathayo 6:5-13

KIONGOZI:

"Ombi la Bwana" ni mfano wa mtindo ambao Yesu alitoa wa kusaidia kujua jinsi ya kuomba. Yesua alitunya tusiwe kama "wanafiki"

(Mathayo 6:5) wanaopenda kuomba wakionekana na watu. Kurudia rudia maneno ya aina moja mara nyingi ni kama kupayuka payuka wala siyo kuomba. Mungu anazijua haja zetu,

hatuombi ili ndipo tumjulisha Mungu haja zetu. Tunaomba ili ndipo tushirikiane na Mungu na kumwonyesha jinsi tunavyomtegemea.

SEHEMU YA KWANZA: "Baba Yetu"

(Soma Mathayo 6:9).

Baba tunayemwomba ndiye Muumba, Mungu wa mbinguni, Mungu wa milele. Ndiye Mungu aliyetwa "Mimi Niko Ambaye Niko." Hatuendi mbele zake Mungu kwa sababu tunafaa au kwa sababu matendo yetu ni mema. Tunamwendea Mungu kwa njia ya maombi na kwa sababu yeye ndiye baba yetu na sisi tu watoto wake.

Baba yetu huishi mbinguni. Yeye hafungwi na vitu vya ulimwengu huu au vitu vya siku hizi. Huyaona mambo yale yatufaayo katika miaka ijayo. Yeye ni Baba mwenye nguvu zote naye anao uweza wa kuzifanya mbingu na nchi "kufanya kazi pamoja na wale wapendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake" (Warumi 8:28).

Zamani za Biblia jina lilieleza hali na tabia za mtu. Jina la Mungu ni takatifu kwa sababu yeye ni mtakatifu. Tunapomba "Jina lako litukuzwe" huwa tunaomba ya kuwa Mungu ataonyesha hali na kusudi lake lililo takatifu. Tunaonyesha kwamba mioyo yetu itamwelekea katika kumsifu.

SEHEMU YA PILI: "Ufalme Wako Uje"

(Soma Mathayo 6:10).

Tunapoyatamka maneno haya tunaomba kuwa ufalme wake Mungu

utimizwe mioyoni mwetu, nyumbani kwetu, katika miji na vijiji vyetu, ndani ya serikali yetu, na katika dunia nzima. Huwa tunamwomba Mungu ayatende mambo yote!

Yesu alisema ya kuwa, "na kwa nini mnaniita, Bwana, walakini hamyatendi nsemayo?" (Luka 6:46). Kule mbinguni mapenzi ya Mungu hutimizwa kikamilifu. Hakuna dhambi wala kuasi kule kunakoharibu amani na utukufu. Wale waaminio katika ufalme wake Kristo huishi maisha ya kuleta ufalme wa mbinguni utawale hapa duniani kama inavyowezekana. Ombi hili silo ahadi tu ya kuyatafuta mapenzi ya Mungu, lakini ni ahadi pia ya kutuongoza kuyafuata mapenzi ya Mungu badala ya kuyafuata mapenzi yetu. Tunaweza kusema kama Yesu, "Walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe" (Mathayo 26:39).

SEHEMU YA TATU: Kuombea Haja za Mtu Binafsi

(Soma Mathayo 6:11-13).

"Utupe leo riziki yetu." Mkate unasimama mahali pa chakula na vitu vingine vinavyohitajika katika maisha yetu. Inafaa sana kumwomba Mungu atupe kitu kile tunachokihitaji kwa sababu jambo hili hudhihirisha kwamba tunamtegemea yeye. Ikiwa yeye hutuma mvua na hung'aza jua, hutupa nguvu za kutuwezesha kufanya kazi, basi atatupa maarifa ya kufanya kazi nzuri. Yeye hutupa riziki zetu za kila siku.

"Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu."

Kusamehe maana yake ni kuondoa, au futilia mbali, au kuachia mbali. Naye Mungu hufanya mambo hayo yote anapotasamehe dhambi zetu. Deni hulipwa. Huwa hatuna deni tena. Tunaomba kwamba Mungu atatusamehe kama vile nasi tunavyowasamehe wale wanaotukosea. Kusamehe ni kusahau, kutenda kana kwamba maneno fulani hayajatamkwa, au matendo fulani hayajatendwa. Hii maana yake ni kusema kuwa hatutalipiza kisasi lakini tutatafuta ushirika wa upatanisho. Tunasamehe kwa sababu "tumesamehewa."

"Usifutie majaribuni lakini utuokoe na yule mwovu." Tunamwomba Mungu atusamehe kushindwa kwetu, makosa yetu pamoja na dhambi zetu. Kwa kujua udhaifu wetu na kuufahamu ulimwengu wenye dhambi ambao tunaishi ndani yake, tunamwomba Mungu atupe nguvu zake ili ndipo atuokoe kutoka kwa yule mwovu (Shetani). Kwa maana

ufalme ni wa Mungu, na nguvu na utukufu ni vya Baba Yetu Aliye Mbinguni.

KIONGOZI

Sasa tuombe tukiwa katika hali ya kuinamisha vichwa vyetu na kugeukia Mungu na mioyo yetu. Turudie ombi la Bwana polepole kwa sauti nyororo kwa sababu ya yale yote ambayo Roho Mtakatifu ametufundisha leo.

*"Baba yetu uliye mbinguni,
Jina lako litukuzwe,
Ufalme wako uje,
Mapenzi yako yatimizwe hapa
duniani kama huko mbinguni
Utupe leo riziki yetu
Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi
tuwasamehevyo wadeni wetu.
Na usitutie majaribuni lakini
utuokoe na yule mwovu
Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu
na utukufu, hata milele
Amina.*

Mpango wa Saba

NJIA, KWELI NA UZIMA

Kilini cha Masomo: Maneno Makuu ya Biblia

Kifungu cha Kukumbuka:

"Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haki kwa Baba, ila kwa njia ya mimi."
Yohana 14:6

Kuyasoma Maandiko: Yohana 14:1-15

KIONGOZI:

Yesu alitaka wanafunzi wake wajue ya kuwa baada ya siku chache watu waovu watamwangamiza Yeye, lakini

Mungu atajitukuzisha na kuyaleta maisha mapya kwa watu wengine kwa sababu ya kifo cha mwanaye. Yesu

Lakini hatuhitaji kukaa na njaa bila kupata chakula. "Nisikilizeni kwa bidii, mle kilicho chema, na kujifurahisha nafsi zenu kwa unono. Tegeni masikio yenu, na kunijia; sikieni, na nafsi zenu zitaishi" (Isaya 55:2-3). Bwana asema hivyo kwa kinywa cha nabii wake. Muda wa miaka mingi baadaye Yesu alisema "Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele" (Yohana 10:10).

SEHEMU YA TATU: "Mtafuteni Bwana,..."

(Soma Isaya 55:6-9). Sehemu ya mwito mkuu wa Mungu ni hiyo ya msamaha. Bwana Mungu yu karibu. Anaweza kupatikana, lakini ni lazima tumtafute na kumwita maadamu tunayo nafasi. Siku ya msamaha inaweza kupita kabla hatujakata shauri kumtafuta Mungu.

Njia ya kumtafuta Bwana ni wazi. Mtu mbaya aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake na "amrudie Bwana" (Isaya 55:7). Watu wengi wamejindanganya kwa kufikiria kuwa kwa maana wameamini sawasawa, hawajali hata wakiishi

maisha ya namna gani. Lakini tunahitaji kubadilisha mawazo na matendo yetu, kisha tumwelekee Mungu. Tukifanya hivyo, Mungu atatuhurumia na kutusamehe kabisa. Kwa mnunuzi kipawa hiki hakimgharimu cho chote, lakini kwa mwuzaji ni cha gharama kuu. Tuisahau ya kuwa Isaya 55 imetanguliwa na Isaya 53, sasa msalaba umesimama katikati ya mpango wake Mungu.

KIONGOZI

Kitu cho chote kitakachotolewa na ulimwengu hakiwezi kututoshelesha kabisa, hata kama kikiwa ni pesa, anasa, sifa, uwezo au utamaduni. Hata tukishiriki katika anasa za ulimwengu namna gani, bado tungali na kitu ndani yetu kinachosema, "Mimi nina njaa. Naona kiu." Kwa nini usikubali mwito wa karamu ambayo inatayarishwa na mfalme. Sasa karamu hiyo iko tayari. Mungu yu karibu. Sasa ndio wakati wa kupata wokovu huo. Yeye yu tayari na anapenda kusamehe sasa. Jitayarishe kuupokea ukombozi leo. Pengine KESHO utachelewa.

Mpango wa Kwanza

HAPO MWANZO

Kiini cha Masomo: Maneno Makuu ya Biblia

Kifungu cha Kukumbuka:

"Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana." Mwanzo 1:31

Maandiko ya Biblia: Mwanzo 1:1 - 2:3

KIONGOZI

Je, ni nani aliyeiumba nchi? Sikuzote watu wamewaza jibu la swali hili ni nini. Wamekata shauri kwamba wanaume au wanawake hawakuweza kuiumba nchi kwa sababu ni kubwa na ya ajabu mno. Mtu fulani ambaye anaye uwezo zaidi ya sisi ndiye aliyeweza kuiumba nchi. Kwa maana watu hawakujua ni nani na ni mtu yupi aliyefanya hivyo, basi walianza kujitungia hadithi kuhusu mtu huyo. Wakati ulimwengu ulipoumbwa hapakuwa na mtu mwingine ila Mungu, aliye mjumba. Lakini siku moja Muumba wa ulimwengu, yaani Mungu wa kweli, aliwaongoza watu kwa njia ya roho wake kuandika habari za uumbaji. Habari hii ya uumbaji imeandikwa kitabu cha kwanza cha Biblia kiitwacho kitabu cha Mwanzo.

SEHEMU YA KWANZA: "Hapo Mwanzo"

Mwandishi wa kitabu cha Mwanzo aliandika kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu kuwa, "Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi" (Mwanzo 1:1). Kifungu hiki cha kwanza ni sehemu ya maana sana ya

Kitabu cha Mwanzo. Ni kweli kwamba Mungu mmoja aliye wa kweli ndiye aliyeiumba, vitu vyote. Ulimwengu haukutukia kwa ghafula au kwa bahati mbaya. Mungu aliuumba ulimwengu kwa neno lake. Neno "Kuumba" linao maana ya kusema kuwa Mungu hakuumba kitu kutoka kwa kitu kingine. Ulimwengu huu ni wake Mungu kwa sababu aliuumba. "Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa" (Ufunuo 4:11).

SEHEMU YA PILI: "Mungu Akasema"

Tangu mwanzo, Mungu alijifunua kama Mungu anayenena. Yeye hunena kwa mamlaka na kwa nguvu. "Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake" (Zaburi 33:6). "Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri" (Waebrania 11:3). "Mungu akasema, Iwe Nuru; ikawa nuru" (Mwanzo 1:3). Kitu cha kwanza ambacho Mungu akitoa kwa

ulimwengu kilikuwa nuru. Nuru hii haikutokana na mwangaza wa jua, mwezi au nyota, kwa maana vitu hivyo havikuumbwa mpaka siku ya nne ilipotimia. Nuru ilikuwa iking'aa kutoka katika mwangaza wake Mungu. Giza lililoifunika nchi liiangaziwa na Mungu. Mungu akiingia, giza hutoroka. Nuru ya Mungu huushinda mwangaza wa jua. "Wala hapatakuwa na usiku tena, wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele" (Ufunuo 22:5).

SEHEMU YA TATU: "Uumbaji Mwema Wake Mungu"

Kabla Mungu hajaumba wanyama na mwanadamu, alikuwa amekwisha tengeneza kila kitu ambacho watahitaji. Siku ya pili aliweka anga nchini ambayo huleta mvua, na hewa na vitu vingine vinavyohitajika na wale aliopanga kuwaumba. Siku ya tatu Mwuumba aliyakusanya maji baharini kukawa na nchi kavu. Mungu akasema kuwe na majani pamoja na miti ya kuwapatia hao viumbe maishilio. Siku ya nne Mungu akazifanya jua, mwezi na nyota ili kuwe na tofauti kati ya usiku na mchana. Akiwa Bwana wa Nyakati, akasema kuwa na majira, siku na miaka. Siku ya tano baada ya kila kitu kufanywa, Mungu akavifanya viumbe vya kufurahia kila kitu alichofanya. Mungu aliwaumba wanyama, nyuni wa angani na kila

aina wa samaki wa majini na kila kitambaacho juu ya nchi.

SEHEMU YA NNE: "Mungu Akaumba Mtu"

Mtu ndiye aliyekuwa lengo na fahari ya uumbaji wote. "Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba" (Mwanzo 1:27). Mtu ni wa maana sana kwa sababu aliumbwa kwa mfano wake Mungu. Mtu aliyecumbwa kwa mfano wake Mungu anaweza kuwaza na kufikiria. Ana uwezo wa kuchagua; ana uwezo wa kujua wajibu wake; ana uwezo kuchukua madaraka; ana uwezo wa kutokuwa mchoyo na kuwa na uhusiano mwema na watu wale wengine. Lakini jambo la maana sana ni hilo ya kuweza kuwa na uhusiano mwema na Mungu. "Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana" (Mwanzo 1:31).

KIONGOZI

Zaburi 100:3 hutuambia, "Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu; ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; tu watu wake, na kondoo wa malisho yake." Mungu ndiye aliyetuumba. Anajua kile kifaacho kwetu. Ebu tuombe maombi ya shukrani kwa sababu ya mambo yake aliyotutenda. Ebu na tumwambie katika maombi kwamba kwa kweli tunataka kuwa wake na kondoo wa malisho yake.

Mpango wa Kumi na Moja

MWALIKO MKUU

Kiini cha Masomo: Maneno Makuu ya Biblia

Kifungu cha Kukumbuka:

"Mtafuteni Bwana, mwanadamu anapatikana, mwiteni, maadamu anapatikana."
Isaya 55:6

Kuyasoma Maandiko: Isaya 55:1-3, 6-9

KIONGOZI:

Isaya 55 iliandikwa hasa kwa Wayahudi walioishi nchi ya Babeli kwa muda wa miaka mingi. Walitekwa nyara wakapelekwa mateka wa vita mpaka nchi ya Babeli. Na kule katika nchi ya uhamisho walianza kufanya kazi ya biashara na uchuuzi. Walisahau kuwa Mungu aliwaita kuwa makuhani. Badala ya kushuhudia habari za Mungu Yehova, waliyafurahia maisha ya kipagani. Waliyatimia maisha yao katika kupata faida ya biashara kuliko kutoa mali zao. Mungu aliwaalika watu wa zamani za Isaya na hata kwetu sisi.

SEHEMU YA KWANZA: Mwaliko kwa Watu Wote

(Soma Isaya 55:1).

Mwaliko ulitolewa kwa wale walio na kiu na wale walio na njaa. Umetolewa kwa watu wale ambao mioyo yao ina haja na inayohitaji kushirikiana na Mungu. Sisi tu maskini wa "kiroho." Rehema yake Mungu haiwezi kubadilishwa wala kununuliwa. Haiwezi kupatikana kwa kuwa na pesa au kwa njia ya matendo. Huwezi kuipata kwa njia ya kufanya

kazi au kuwa na haki ya kuipata. Mungu hutoa kipawa hicho bure, ndicho Mungu mwenyewe. Ni lazima tumwendee na kupokea kila alichacho nacho kwa ajili yetu.

Kile Mungu alichotupa hututosheleza. Hutoa kwa ukarimu. Divai na maziwa au mkate na mafuta ndiyo maneno yale yanayotumiwa katika kuonyesha utajiri wa maisha ambayo hupatikana mtu akiwa pamoja na Mungu. Vitu hivyo husimama mahali pa wingi wa baraka wanazozipata wale wanaoingia katika ufalme wa Mungu.

SEHEMU YA PILI: Mkate Ambao Haushibishi

(Soma Isaya 55:2-3).

Wale ambao wanatafuta kitu cha kushibisha nafsi zao wanafananishwa na watu wanaotumia pesa zao kununua mkate usioshibisha. Siku hizi kama ilivyokuwa zamani za Isaya, watu wengi huabudu sanamu na miungu wa uongo, wakijaribu kutafuta kushibishwa. Watu wengi hutafuta anasa, uongozi, cheo au sifa za kushibisha nafsi zao.